

**KENYA HIGH SCHOOL**  
**MOCK 2019**  
**KISWAHILI PAPER 3**

**SEHEMU A : FASIHI SIMULIZI**

1. lazima  
(a) Miviga ni nini? (alama 2)
- (b) Eleza sifa tano za Miviga (alama 5)
- (c) Fafanua hasara tatu za miviga (alama 3)
- (d) Eleza changamoto tano ambazo mtafiti hukabiliana nazo anpokusanya data ya miviga (alama 10)

**SEHEMU B:**  
**TAMTHLIA – Kigogo (Pauline Kea)**

2. Onyesha namna mwandishi alivyofanikiwa kukuza maudhui yafuatayo
- (i) Elimu (alama 10)
- (ii) Ujana (alama 10)
3. Mvunja nchi ni mwananchi 'Eleza ukweli wa kauli hii kwa kurejelea matukio katika tamthlia ya kigogo (alama 20)

**SEHEMU YA C: USHAIRI**

B: Moyo wanambia imba, dikteta simwimbie  
Moyo Wanambia lumba, muhitaji mlumbie  
Moyo wanambia chimba, maovu uyachimbue  
Moyo wanambia woga, ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia kuwa, ila kasuku usiwe  
Moyo Wanambia iwa, kunguni ila usiwe  
Moyo wanambia pewa, cha mnyonge usipewe  
Moyo wanambia woga, ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia nenda, penye dhuluma senende  
Moyo Wanambia penda, mnyonyaji simpende  
Moyo wanambia ponda, ateswaye simponde  
Moyo wanambia woga, ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia tenda, lenye jamala litende  
Moyo Wanambia unda, lenye faida liunde  
Moyo wanambia tunda, lisilo sumu litunde  
Moyo wanambia woga, ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia ota, kuwa mwizi usiote  
Moyo Wanambia kata, marija yote ikate  
Moyo wanambia teta, penye dhuluma patete  
Moyo wanambia woga, ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia nyosha, penye na kombo panyoshe  
Moyo Wanambia usha, mateso yote yaushie  
Moyo wanambia isha, penye majonzi yaishe  
Moyo wanambia woga, ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia waza, yalopita yawazie  
Moyo Wanambia kaza, mwovu njia mkazie  
Moyo wanambia vuaza, lenye heri tuyazie  
Moyo wanambia woga, ndio mwazo wa maafa

*(Shairi la mbegu la E. Kezilahabi, 1988)*

- (a) Fafanua dhamira ya mtunzi wa shairi hili ( alama 2)
- (b) Ainisha bahari za ushauri huu kwa kutegemea
- (i) Mpangilio wa maneno
- (ii) Vipande vya mishororo
- (iii) Idadi ya mishororo kwa kila ubeti ( alama3)
- (c) Tambua aina moja ya urudiaji na utolee mfano ( alama 2)
- (d) changua muundo wa shairi hili ( alama 4)
- (e) Andika ubeti wa tano kwa lugha ya nathari ( alama 4)
- (g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika ushairi (alama 2)
- (i) Dikteka
- (ii) Kasuku

(iii) Mnyonyaji

**USHAIRI**

Ni mimi nizamishaye chini  
Mizizi kwenye majabali  
Kufyonza chumyi!

Ni mimi ninyunyizae maji  
Ili mimea ifumbue  
Nafasi zao hewani  
Ili miti ishike mimba kuzaa  
Matunda,nafaka,mizizi na viazi  
Ela mimi sili hata punje moja  
Nabaki mtupu!

Ni mimi tumbo kubwa,  
Niliyeshiba madini  
Ni mimi ninayechimba  
Kupakua raslimali

Dhahabu,chuma,makaa...

ela yote yanaona  
Yatiririka kwao!  
Nabaki mtupu!  
Vyakula vyote nazalisha mimi  
Na mi' nabaki na njaa!

Nguo zote nawapa mimi  
Na mi' nabaki u tupu!

Madini yote nawapa mimi  
Na mi' nabaki kununua vyao!

Kazi zote nafanya mimi  
Wao wabaki kunila nguvu!

Wao wanajita bora  
Na mi' nabaki fukara!

(Shairi la S.A Mohamed Jicho la ndani, Longhorn Publishers 2002)

- (a) Lipatie shairi hili anwani mwafaka (alama 2)
- (b) Fafanua aina moja ya taswira katika shairi hili (alama 2)
- (c) Eleza ujumbe mkuu wa mtunzi wa shairi hili (alama 2)
- (d) Huu ni ushairi wa aina gani. Toa sababu ya jibu lako (alama 2)
- (e) Eleza toni ya ushairi (alama 2)
- (f) Mtunzi ametumia mbinu zipi kukuza ujumbe wake (alama 4)
- (g) Huku ukitolea mifano onyesha matumizi ya mistari mishata katika shairi hili (alama 2)
- (h) Onyesha u muhimu wa kinaya katika shairi hili (alama 2)
- (i) Tambua nafsi neni katika shairi hili (alama 2)

**SEHEMU D:**

**Hadithi fupi (Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine)**

6 Onyesha namna nafasi ya mwanamke inavyosawiriwa kwa kuzingatia hadithi zifuatazo

- (a) Ndoto ya mashaka
- (b) Masharti ya kisasa
- (c) Mapenzi ya kifaurongo
- (d) Shogake dada ana ndevu

7. ....Ati umebakwa! nani akubake wewe? Wapi utakapobakwa mji pasiwe na mtu wa kukuombea?

- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
- (b) Eleza sifa mbili na umuhimu wa msemaji wa maneno haya (alama 4)
- (c) Jadili maudhui makuu katika dondoo hili (alama 12 (6 x 2))

**SEHEMU YA E:**

**Chozi la Heri**

(alama 20)

8. Jadili ufaafu wa anwani chozi la Heri.